

Title: Anita Varney – Health Facilitator, Fishtown/Liberia
Author: Stefanie Duckstein, HA Afrika/ Nahost
Editor: Christine Harjes
Translator: Tony Dunham
Sound Clips in DALET: Learning by Ear:
LbE_PEO_Liberia_Varney

Characters

Narrator: Male voice
Voice Over: Anita Varney, 36

INTRO

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako juu ya Watu Wanaoleta Maendeleo katika jamii. Leo hii tunakutana na Anita. Yeye ni muhudumu wa afya katika eneo la kijijini kwenye nchi moja ya Afrika Magharibi. Kwa hivyo tunakwenda moja kwa moja hadi mji mdogo wa Fishtown, nchini Liberia.

1. SFX: Women's Workshop

Ab: 0:48: Anita: "kina mama oh kina mama. (Clapping hands) Umeme, Umeme. Ni maambukizi ya ugonjwa wa zinaa. Gonorrhoea.

All: Gonorrhoea.

Anita: Syphilis.

All: Syphilis

Anita: Mnamalizia wenyewe ...Vizuri!"

Mchana wa leo wanaburudika juu ya kilima kimoja kati ya vilima vitatu vinavyounganisha kijiji cha Fishtown. Majina ya magonjwa ya kuambukiza kutokana na ngono yanatajwa mle ndani ya chumba huku sauti hizo zikisika hadi nje uwanjani. Anita hatulii mguu mmoja huku mwingine kule, na anajaribu licha ya joto kali kuwatuliza wanawake wale 30 ili wamsikilize.

2. SFX: Women's Workshop

Anita anaashiria kwa kidole chake, picha za sehemu za siri zilizoathirika. Wanawake wanajisogeza kwenye viti vyao huku wakiguna kwa sauti za chini. Mada ya warsha ya leo ni magonjwa ya zinaa. Sio mada ya kupendeza sana, kwa mujibu wa Anita – “Kwa hivyo usipowachangamsha, watachoka.”

3. SFX: Women's Workshop

Anita Yawasese Varney, urefu wake ni kama mita moja na sentimita themanini hivi, ni mrefu kuliko wanawake wote hapo. Hata mwili wake ni mkubwa kuliko wengine. Anapenda kuvaa viatu vya spoti na suruali ya jeans inayombana, wakati wote simu yake ya mkononi huwa inaning'inia kwenye mkanda wake. Anita ana miaka 36, yeye ni mkunga na mshauri wa maswala ya afya wa shirika la Medica Mondiale, shirika la Kijerumani la kutetea haki za wanawake. Shirika hili lilijenga ofisi yake ndogo katika kijiji cha Fishtown. “Wanawake na wasichana hukabiliwa na hali ngumu nchini mwao,” anasema Anita huku akiwapa mikono na kuagana na wasichana wanaoondoka.

4. Sound Clip Anita, Eng.

„Wanaawake wa Afrika tunapenda kuamini kuwa wanawake ni kama vitu tu katika nyumba zao. Yaani wao wameumbwa kusema ndio Bwana kila wakati kwa waume zao. Hawana haki ya kutoa mapendekezo. Kwa sababu wanaume wanajiona kuwa wao ndio majogoo, wanaofaa kuwika. Wanatawala nyumba zao, mpaka maisha ya wake zao.”

Kwa mujibu wa Anita, jambo hilo halifai kukubalika. Anatingisha kichwa chake na kuweka mikono yake kiunoni.

5. Sound Clip Anita

„Ndio maana tunapambana. Tunajaribu kueneza elimu juu ya haki za binadamu ili kuwafanya wanawake wakubalike katika jamii kama wenza na sio wake tu wa kupigwapigwa au kutumiwa vibaya nyumbani, yaani kuwa kama vitu mbele ya waume zao na sio watu.”

Vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Liberia vilichukua miaka 14 hadi kumalizika. Kwa mujibu wa Medica Mondiale wanawake wawili kati ya wanawake watatu walibakwa. Wakiwemo watoto wadogo na wanawake wazee. Wengi kati ya wanawake hao walitekwa nyara na kulazimishwa kuwa wanajeshi au kufanya kazi ya ukahaba. Hata baada ya vita kumalizika hapo mwaka 2003, visa vya utumiaji nguvu havikuishia hapo. Anita anasema kuwa ipo haja ya kusisitiza heshima miongoni mwa wanaume na wanawake na hatua hiyo ifuatiliwe polepole, hatua kwa hatua.

6. Sound Clip: Anita

„Ni mapambano: wanaume wanapata hofu iwapo wanawake watachukua madaraka, wanafikiri labda watanyag'anywa kabisa ufalme wao. Kwa hiyo kuna mvutano mkubwa kati ya wanaume na wanawake. Lakini lazima wakubali vita hivyo, taratibu tumeanza kuona matunda. Wanaume wameanza kukubali kuwa wanawake ni wenzi wao na wana uwezo wa kutoa michango yenye faida iwapo watapewa nafasi.”

7. SFX: Road Fishtown

Waliberia wanapenda kusema kuwa hakuna chochote cha maana katika kijiji cha Fishtown, wanatania kwamba hakuna hata samaki kama jina la mji huo linavyoamaanisha kwa lugha ya kimombo. Hata wale wanaoishi huko nao husema hivyo hivyo. Lakini hiyo yote sio kweli. Wenyeji wa huko wameuchimba mji huo mdogo katika eneo la Kusini mashariki mwa Liberia kutoka kwenye msitu mnene. Barabara ya udongo inagawa eneo hilo kati ya magharibi

na mashariki. Siku ya soko ambayo ni kila siku ya Alhamisi, mirundo ya samaki waliokaushwa huuzwa. Si hayo tu, mji mdogo wa Fishtown una ukumbi, kiwanja cha mpira, kituo cha polisi na pia maduka machache bila kusahau vilima vitatu vinavyokamilisha mpaka wa mji huo mdogo.

8. Sound Clip: Anita

„Oh Kilima,... ninakizungumzia kilima hiki huku nakipanda. Kwa hiyo pumzi zinaniishia. Tafadhali. (Laughs).”

Anita anapanda kilima kuelekea nyumbani kwa Luise Kwe. Jezi ya rangi ya manjano imeanikwa juani. Mjukuu wa Luise anachapa maji ndani ya beseni la plastiki. Luise anatuashiria tuingie ndani ya chumba chenye kuta ambazo zimejengwa kwa kutumia vifaa vya ujenzi vya kale. Kwa haraka anatafuta kitabu chake cha kumbukumbu ambacho amenakili kila mtoto aliyezaliwa na safari alizofanya majumbani.

9. SFX: Luise house

Luise ni mmoja kati ya wakunga wengi wa kienyeji. Alijifunza kazi hiyo ya kuwasaidia akinamama wajawazito wakati wanapojifungua kutoka kwa mama yake na pia kutoka kwenye kozi moja ya Anita ambayo alihudhuria. Luise amesaidia kuwaleta watoto wengi wa Liberia duniani katika umri wake wa miaka 62. Anita hufika iwapo kuna matatizo na Luise anapokuwa hajui la kufanya. Ni jana tu anasema Luise huku uso wake ukionyesha woga, Ni jana tu alilazimika kumpeleka jirani yake kliniki. Alipatwa na maumivu makali. Anita anafuatilia kwa makini shughuli za Luise, hutaka

kujua juu ya afya ya mama mja mzito na vipimo vya mimba pamoja na hali ya mtoto aliye tumboni kwa jumla.

10. Sound Clip Anita:

„Kufanya kazi ya kutoa huduma kwa jamii, sio kwamba wewe uko juu na jamii iako chini yako, hapana ni lazima ujumuike pamoja na watu, ni muhimu kukubali hali yao ya maisha ndio na wao watakukubali. Lakini ukijaribu kujifanya kuwa wewe ni tafauti, au wewe ni mtaalamu ama mtu mashuhuri basi hautakubalika hata kidogo. Na ujumbe unaojaribu kuufikisha kwa jamii hautafika kamwe. Kwa hivyo ukikuta wao wanakaa chini kwenye sakafu basi na wewe kaa nao, hata ukiletewa kiti kataa ili kuwaonyesha kuwa wewe na wao mko sawa.“

Sio jambo rahisi, anasema Anita, huku akijitoa ukope kwenye jicho lake.

11. Sound Clip Anita

„Kwangu mimi hii ni changamoto kubwa katika kazi yangu ya kutoa ushauri katika maswala ya afya na vilevile kama mwanamke niliyeolewa. Nina mume na nina watoto watatu. Mume wangu yuko Monrovia. Anaishi na watoto wetu kule. Shida niliyo nayo ni kuwa mume wangu analalamika saa zote: anasema lazima uje nyumbani ulee watoto hakuna mtu anayewapa malezi ya mama, watoto wanahitaji kuonyeshwa upendo, wanakuhitaji. Huwezi kuwageuzia mgongo na kujali kazi yako tu. Yaani analalamika wakati wote. Inabidi nimueleweshe ili niweze kuendelea na kazi yangu.“

Wakati hamu kubwa ya kumuona mumewe na watoto wao, Joel, Francis na Franita ikimjia, yeye hutumia usafiri wa kawaida kwa siku mbili hadi katika mji mkuu wa Monrovia. Maisha ni mazuri kule. Huduma za afya ni bora, watu wanajihusisha na mambo mengi. Kuna hata sinema mjini Monrovia. Lakini hayo si muhimu kwake kwani mawazo yake hufikiri tu juu ya mji mdogo wa Fishtown na kukumbuka kuwa wakati ule anahitajika zaidi.

12. Sound Clip Anita

„Kutokea mwanzo mimi sikuwa muhudumu wa afya. Nilikuwa Anita tu kutoka shule ya upili. Nilikuwa nina ndoto hii ambayo nilitaka niitimize. Shabaha yoyote uliyonayo maishani unaweza kuitekeleza, inategemea na wewe mwenyewe tu, bidii yako na uvumilivu. Kwa hivyo Anita niko sawa na mwanamke mwingine yeyote anayeweza kutimiza lengo lake maishani. Ninawahimiza wanawake; wanaweza kabisa kufikia malengo yao na kuwa msaada mkubwa katika maisha ya watu wanaohitaji msaada huo. Na hilo ndilo jambo la muhimu. Ukimsaidia mtu maisha yako hayatakuwa kazi bure. Nina amini hilo sana.”

13. SFX Anita walking

14. SFX thunder storm

Upepo unatetemesha mabati. Kutoka mashariki msimu wa mvua umeanza. Anita anaelekea katika hospitali ya mji wa Fishtown. Wizara ya afya ya Liberia ina nyumba yenye vyumba vitatu vidogo vya wagonjwa, maabara na chumba cha kujifungulia kina mama wajawazito, nyumba hiyo imepakwa rangi ya kijani na nyeupe. Nyumba hiyo ni hospitalli. Friji la kuwekea dawa linafanya kazi kwa nguvu ya jenereta inayonguruma kwa sauti kubwa. Anita anapita kati ya kundi la wasichana. Nguo zao zimetunishwa na matumbo yao ya duara. Anita anageuka na kusimama mbele ya kundi hilo halafu anateremsha mabega yake.

15. Sound Clip Anita

„Habari za asubuhi nyote. Saa tatu 3:00 Na leo hii tutazungumza juu ya: Kuwatunza watoto wetu, wote: „kuwatunza watoto wetu.”

Kwa maelezo ya kina yanayoeleweka, Anita anatilia mkazo umuhimu wa chakula chenye vitamini za kutosha. Matunda mengi, mboga na maji safi ya kunywa. Wanawake wanafuatilia maelezo yake kwa shauku.

16.SFX: Training at Clinic

Baada ya kipindi cha chini ya dakika 30, tayari Anita anakimbilia miadi yake inayofuata. Katika chumba cha mwisho ndani ya kliniki hiyo Martha anatandika shuka nzuri za rangi, amechoka lakini ana furaha. Alijifungua jana usiku. Mtoto wake wa saba. Ijapokuwa hii ndio mimba yake ya kwanza yeye kujifungua katika kliniki.

17.SFX: Anita talking to mother

Akiwa njiani kuelekea nyumbani, Anita pia anahisi uchovu kidogo. Tabu za wanawake nchini mwake huwa zinamuangukia yeye mara nyingine yeye husema hivyo. Inawabidi kupambana na mambo mengi tofauti. Chakula mara nyingi kinakuwa ni cha aina moja hakuna mabadiliko, maji ya kunywa si safi. Lakini baya zaidi ni manyanyaso ya kimwili. Ubakaji ndani ya familia unafanyika kila mara. Shirika la Medica Mondiale limempa mafunzo ya kukabiliana na hayo yote kiakili ili aweze kuwasaidia wanawake ambao wana matatizo kutokana na dhulma na mateso yaliyowafika. Lakini sio kazi rahisi hata kidogo.

18. Sound Clip Anita

„Hmm. Whoa. Mara nyingine unakabiliwa na ugumu hasa pale unapokumbana na kisa ambacho hata binadamu yeyote hangeweza kudhani kuwa kisa kama hicho kinaweza kutokea. Kwa mfano itokee mwanamume amembaka mtoto mdogo. Kesi kama hizo huwa zinaniletea bughdha kubwa. Ninajaribu kutambua njia zikazonipa utulivu. Mojawapo ni kukubali kuwa mambo kama hayo hutokea. Ni sehemu ya maisha. Kilichofanyika huwezi kukibadili. Kwa hivyo cha muhimu ni kukubali hoja halafu kuifanyia kazi. Kwa sababu ukiendelea kukana, mambo hayo huwezi kuyaelewa na kukubali jinsi...”

Shirika la Kijerumani la Medica Mondiale linafanya kazi inayoonekana. Muasisi wake, Monika Hauser, alitunukiwa tuzo ya Muongozo wa Maisha - (the Right Livelihood Award) mwaka 2008. Na hivyo basi Anita alipata fursa ya kupaa angani hadi nchini Sweden kuhudhuria sherehe za kupokea tuzo hiyo katika mji wa Stockholm. Ilikuwa ni mara yake kwanza kulikanyaga bara Ulaya. Anita anayapiga mapaja yake kwa makofi. Anacheka kila anapokumbuka sherehe hizo.

19. Sound Clip Anita

„Nilivaa vazi langu la Kiafrika, kandambili za Kiafrika na nywele zangu nilizitengeneza pia mtindo wa Kiafrika. Nilipendeza sana hata wenyeji wa huko walipendezwa na mavazi yangu kwa sababu si kawaida wao kuona vazi kama lile. Wengi walinifuata na kutaka kupiga picha nami, walikuwa wakisema :Naweza kupiga picha na wewe yaani umependeza sana. Oh. Mungu wangu. (Laughs). Na urefu wangu huu, nilikuwa nawaangalia wote vichwani. Nywele zangu ziliwaziba wale waliokuwa wamekaa nyuma yangu wakati wa sherehe, Jamaa mmoja alikuja na kuniambia nakupongeza kwa kupendeza lakini nashukuru sikuwa nimekaa nyuma yako kwa sababu nisingeweza kuona chochote.” (Laughs)

OUTRO

Je umeifurahia hadithi hii? Iwapo ungependa kutoa maoni yako, soma zaidi kuhusu mada hii au sikiliza tena hadithi hii ya Anita kwenye mtandao. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Asante sana kwa kutusikiliza, ni matumaini yangu kuwa utajiunga nasi tena wakati ujao katika hadithi nyingine mpya kwenye makala haya ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, kuhusu Watu Wanaoleta Mabadiliko. Hadi wakati huo, Kwaheri!

END
